OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NGARA

SHULE YA SEKONDARI LUKOLE,
S.L.P. 41,
NGARA.

14/05/2018.

SIMU: 0784809315/0754710936 MKUU WA SHULE
O783 230123 MAKAMU MKUU WA SHULE
0756279126 MATRON

Kumb. Na. LUK.SS/UT/06/13/……..

MWANAFUNZI ..……
S.L.P. ……
……

YAH: MAAGIZO MUHIMU YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI LUKOLE MWAKA 2018/2019

1.0 Ninafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha V katika shule hii kwa mwaka 2017 tahasusi **ya HGL,HGK,HKL,HGE,CBG na EGM**, Shule ya sekondari LUKOLE ipo umbali wa Km 15 kutoka mji mkuu wa Wilaya ya Ngara. Kutoka kituo cha mabasi Ngara mjini nauli ni sh 2000/= mpaka shuleni hapa.

2.0 Shule iko eneo linaloitwa K9 ni karibu sana na barabara. Kwa wanafunzi wanaotokea maeneo ya Mwanza, Bukoba, Karagwe na Kahama washukie katika kituo cha mabasi cha K9 na hapo watakiona kibao cha shule, ni 50M tu kutoka katika kituo hicho.

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe **02/07/2018** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **01/07/2018, na masomo yataanza mara tu baada ya shule kufunguliwa;** mwisho wa kuripoti ni tarehe **16/07/2018**

3.0 **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

3:1 SARE YA SHULE

a) Sare ya shule hii ni **shati jeupe lenye mikono mirefu**, liwekewe alama ya V kwenye mabega yote kwa kutumia kitambaa cha suruali. Suruali mbili za dark blue vipimo upana kwa chini 18”-20’’ iwe na mfuko mmoja nyuma ,modo haziruhusiwi kabisa, viatu vyeusi vya ngozi vyenye kisigino kifupi vya kufunga na kamba na soksi kwa wavulana. Tai yenye nembo ya shule inapatikana shuleni kwa gharama ya Tsh.3000/= tu aina nyingine ya tai haitaruhusiwa kuvaliwa shuleni.

b) **Shati mbili nyeupe zenye mikono mirefu** zilizowekewa alama V kwenye mabega yote kwa kutumia kitambaa cha sketi. Sketi ya dark blue yenye Linda box (V) Kwa mbele. Sketi iwe ndefu kuvuka magoti., viatu vyeusi vya ngozi vyenye kisigino kifupi na vyenye kufungwa na kamba, soksi

ndefu nyeupe kwa wasichana . Tai yenye nembo ya shule inapatikana shuleni kwa gharama ya Tsh.3000/= tu aina nyingine ya tai haitaruhusiwa kuvaliwa shuleni.

c) Rangi ya Hijabu ifanane na sare ya shule kwa wasichana wa kiisilamu watakaopenda kuvaa Hijabu.

d) **Sare ya baada ya masomo**.

i) Wavulana wanatakiwa kuvaa **T-Shirt rangi ya kijivu** na **Suruali ya rangi ya damu ya mzee** (**T – Shirt** zilizoandaliwa kama unifomu baada ya saa za darasani na zenye nembo ya shule zipo shuleni kwa gharama ya Tshs 15,000/= (SHAMBA DRESS).

ii) Wasichana wanatakiwa kuwa na T shirt kama za wavulana (Tshirt zinapatikana shuleni kwa gharama ya Tshs 15,000/= (SHAMBA DRESS), pamoja na gauni la rangi ya purple ashoneshe mwenyewe **(mshono wa solo**).
Sare ya michezo ni tracksuit ya blue kwa wavula na wasichana.

iii) Sweta ya rangi ya **Zambarau**. Kumbuka kuwa aina nyingine ya sweta au jaketi hairuhusiwi kuvaliwa shuleni na hata nje ya shule kwa muda wote mwanafunzi awapo shuleni. (Sweta ulete mwenyewe).Usipoipata utaikuta shuleni kwa makubaliano yako na muuzaji mwenyewe.

NB: Maeneo haya yana baridi sana hivyo sweta ni lazima.

3.2 **ADA NA MICHANGO YA SHULE**:

(a) Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi 70,000/= (elfu sabini) .
Unatakiwa kulipa kiasi cha Tshs. 35,000/= (thelathini na tano elfu) kwa muhula au zote 70,000/= (elfu sabini) kwa wakati mmoja.

(b) Michango mingine ni kama ifuatavyo:-

i. Samani 15,000/=
ii. Taaluma 20,000/=
iii. Ukarabati 20,000/=
iv. Upishi, ulinzi na wafanyakazi wote wa shule 30,000/=
v. Matibabu 10,000/=
vi. Kitambulisho 6000/=
vii. Nembo ya shule 2000/=
viii. Tahadhari 5000/= (haitarejeshwa)
ix. Mitihani ya kujipima (Mock) 20,000/=Kwa kidato cha sita
x. Bima ya afya (CHF) tsh 5000/= (kama hana bima ya afya)

Kumbuka; fedha zote hizi za **ada na michango mingine**, zote ziwekwe kwenye Account ya shule yenye jina la **LUKOLE SECONDARY SCHOOL CAPITATION GRANT AC. NO. 32101200054** Tawi lolote la NMB, na mwanafunzi alete risiti iliyotumika kuwekea fedha hizi bank na iwe na jina lake. Mwanafunzi asiyeleta bank pay in slip hatapokelewa. Shule haipokei fedha taslimu.Aidha kwa wale wanaolipiwa na wafadhili wakumbuke kuleta uthibitisho wa maandishi yanayoonyesha aina ya malipo watakayolipiwa na yatalipwa lini.

3.3 VIFAA VYA USAFI

i) Ndoo, beseni
ii) Mfagio wa chepeo .
iii) Fyekeo na cicle (kotama)
iv) Rubber squizer/soft bloom

NB; VYOTE NI LAZIMA VILETWE.

3.4 **VIFAA VYA KULALIA**

i) Godoro la 2 ½ x 6
ii) Shuka 2 za rangi ya pinki
iii) Blanket 1, ni lazima kwa sababu eneo hili kuna baridi

3.5 VIFAA VYA CHAKULA

i) Sahani
ii) Bakuli
iii) Kijiko
iv) Kikombe cha ½ lita cha plastiki

3.6 VIFAA VYA DARASANI

i) Counter book 6
ii) Karamu za kutosha
iii) Mwanafunzi **wa HGE/ CBG/ EGM** awe na scientific calculator, mathematical set Na Dissecting kit kwa wanafunzi **wa CBG**
iv) Wanafunzi wa HGL na HKL waje na Oxford Advanced learners Dictionary kwa kila mmoja

3.7 Uje na vifaa vyako vya matumizi ya kila siku kama vile taulo, dawa za mswaki, sabuni za kuogea na kufulia, mafuta nk. Ni vyema pia ukaja na sanduku la mbao au la bati kwa ajili ya kutunzia vifaa vyako. **Kumbuka nguo za kiraia ambazo si uniform za shule na ambazo hazikutajwa zisiletwe na kuvaliwa shuleni.**

3.8 Uje na rimu 1 ya karatasi (photocopy paper (A4)) kwa ajili ya majaribio ya mara kwa Mara.

3.8 uje na picha(PASSPORT SIZE) 4.

4.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII:

4.1 Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini, unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:-

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wenzako na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
b) Mahudhurio mazuri katika shughuli ndani na nje ya shule.
c) Kuhudhuria masomo ya jioni (preparation).
d) Kuwahi katika shughuli za shule.
e) Kuwepo ndani ya mipaka ya shule wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
i) Huruhusiwi Kumiliki simu shuleni

4.2 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UFUKUZWE SHULE.

1. Wizi
2. Kutouhudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/ utoro
3. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
4. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ walezi na jamii kwa ujumla
5. Uasherati , ushoga, usagaji na Ubakaji.
6. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika/ Kunyoa kwa mtindo usiokubalika
7. Kufuga ndevevu
8. Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya kama vile bangi, cocaine, mirungi, kubeli nk.
9. Kupigana wanafunzi kwa wanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yoyote yule
10. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
11. Kudharau Bendera ya Taifa.
12. Kuoa au kuolewa
13. Kupata mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule.
14. Kutoa mimba.
15. Kukataa adhabu kwa makusudi

16. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
17. Kutoroka au kuwa nje ya mipaka ya shule bila idhini ya uongozi.
18. Kufanya jaribio la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
19. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.

5. MAMBO MENGINE MUHIMU

(i) Fomu ya Medical examination imeambatanishwa ijazwe na mganga mkuu wa hospitali ya serikali na ikabidhiwe mara tu unaporipoti shuleni.

(ii) Fomu ya maelezo binafsi ya mwanafunzi mkataba na kutoshiriki katika migomo fujo na makosa ya jinai. Fomu hii inakipengele cha mzazi kukiri, kukubaliana na sheria, kanuni na ulipaji wa ada, michango mingine na maelekezo mengine yatokanayo na shule.

5.0 Tafadhali soma kwa makini maagizo/maelekezo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA LUKOLE

……

ARON DISHON SEKAZOYA

MKUU WA SHULE

FOMU HII IJAZWE NA IREJESHWE SHULENI

Mimi (Jina la mwanafunzi) ……

Naahidi kuwa mtiifu na kutii sheria na kanuni zote za shule. Sitashiriki katika vitendo viovu kwa muda wote nitakao kuwa shuleni.

Mfano: **Migomo, fujo ,makosa ya jinai** nk.

Sahihi ……..(mwanafunzi) Tarehe ……

Mimi (Jina la mzazi) ……..

Nakiri kusoma maelekezo yote na masharti ya shule, nakubaliana na sheria, kanuni, kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

Sahihi …… (Mzazi) Simu …… Tarehe ……..

Namba za simu za watu walio karibu na mwanafunzi

(i) Jina …… No. Simu …….. Uhusiano …..**BABA.**

(ii) Jina …… No. Simu …….. Uhusiano **…..MAMA**

(iii)

(iii) Jina……..No. Simu……..Uhusiano…**MLEZI**

MEDICAL CERTIFICATE

DATE ……
STUDENT'S NAME ……

(NAME IN FULL)

THE MEDICAL OFFICER:
……
……..
……..

I have examined the above named and consider that he/she is physical *fit and mentally*fit/for a full time students. The examination has included the following categories:

I.

(a) Eye – sight ……..
(b) Hearing …….
(c) Limbs …….
(d) Venereal diseases ……..
(e) Epilepsy ……
(f) Leprosy …….

II. Neuroses …….
III. Other serious Diseases ……
IV. Pregnancy ……

Date …… Signature ……

Station …… Designation ……